



LOWELL HIGH SCHOOL

MPANGO WA MAFUNZO YA MBALI

(Imesasishwa 4/7/20 toleo 2.0)

Hati hii inaongoza wanafunzi, familia, wafanyikazi wa shule na walimu katika huduma ya mafunzo ya mbali na matarajio ya LHS katika kufungwa kwa shule kwa sababu ya janga la COVID-19. Wanafunzi na familia watapokea mwongozo kuhusu teknolojia, matokeo, na matarajio katika kazi za shule wakati hatuko shuleni. Habari kuhusu namna ya kuwasiliana na walimu na wasimamizi imo katika hati hii. Tutaendelea kusasisha mpango huu inapohitajika, tafadhali tembelea tena mara kwa mara ili kupata habari sasa.

Mpango wa mafunzo ya mbali ya Lowell High School imepangwa kupatia wanafunzi fursa ili kuhisi muungano na kuongezea masomo yao wakati hawako katika shule ya LHS. Wanafunzi watajikusha na mafunzo na watakariri ustadi muhimu za kielimu katika mchanganyiko wa shughuli za mafunzo yanayosimamiwa na mwalimu na masomo yanayosimamiwa na mwanafunzi. Wafanyikazi wa LHS watawapatia wanafunzi kazi za nyumbani zinazoimarisha na kupanua ustadi muhimu wa kielimu. Wanafunzi wanatarajiwa kukamilisha kazi hizi za nyumba na kuwasiliana kwa utaratibu na walimu wao ili kugawa mafunzo yao na kupokea maoni ya walimu na usaidizi. Matokeo yatatolewa katika msingi wa mraba uliyo hapa chini.

TAHADHARI WANAFUNZI: Iwapo una hali inayokuzuia kutekeleza mpango huu wa mafunzo ya mbali, tafadhali wasiliana/tuma barua pepe kwa ofisi ya nyumba yako haraka iwezekanavyo. Angalia ukurasa wa kwanza katika tovuti ya [LHS website](#) kwa barua pepe za walimu na taarifa ya mawasiliano.

KWA WANAFUNZI NA FAMILIA

NINAFAA KUFANYA NINI KWA MAFUNZO YA MBALI?

- Wanafunzi wanahitaji simu mahiri, Chromebook, kipakatalishi, Kompyuta, au Tablet. Wanafunzi wote walifanyiwa utafiti kuhusu mahitaji ya mashine ya kutumia kwa mtandao ili kujihusisha na shughuli hii. Wale waliojibu utafiti wakiwa na mahitaji yaliyo na hati wamepatiwa mashine ya kutumia. Ni muhimu kujua kwamba tumeamuru ya kwamba maagizo yaweze kupatikana katika simu pamoja na kompyuta. Inatakiwa kuweza kufanya kazi hizi zote kupitia simu mahiri. Tunaelewa kwamba wanafunzi wengi hufanya hivyo na kwa hivyo hili litawezesha upatikanaji bora zaidi kwa wanafunzi wetu wote.
- Wanafunzi watahitaji [Upatikanaji wa mtandao](#) kwa programu wanazotumia walimu, ambazo zinaweza kuwa kati ya yafuatayo:
 - Google Classroom na Google Apps for Education
 - Akaunti ya mwanafunzi ya baruapepe ya shule
 - Aspen Portal
 - Tovuti binafsi ya walimu (zilizo na za simu)
 - Programu zinginezo za mawasiliano zinazotumiwa na walimu kama: Remind, Zoom, Twitter, Facebook
- Uwezo wa kutumia Aspen Portal
 - Wanafunzi wanaohitaji kuweka upya kwa kifunguo chao cha siri wanafaa kutuma baruapepe kwa aspenportal@lowell.k12.ma.us wakitumia baruapepe yao ya shule.
 - Wanafunzi wanaohitaji kuingia akaunti ya watoto wao wanafaa kutuma barua pepe kwa aspenportal@lowell.k12.ma.us pamoja na jina la kwanza na la mwisho la mtoto wao.
- Baruapepe ya shule (katika programu ya Google Classrooms)
 - Wanafunzi wanafaa kutumia akaunti zao za shule ili kutekeleza shughuli za shule.
 - Wanafunzi wanafaa kuangalia akaunti zao za baruapepe ya shule kwa utaratibu siku za Jumatatu na siku zingine.
 - Walimu, Ofisi za Nyumba, na Wafanyikazi wa Shule watatumia akaunti za baruapepe za shule ili kuwasiliana na wanafunzi inapofaa.
 - [Baruapepe za Walimu](#) huweza kupatikana katika ukurasa wa kwanza wa tovuti letu au unaweza kuonekana katika Aspen Portal haswa katika sehemu la Elimu.

MATARAJIO YA WANAFUNZI:

- Wanafunzi wanatarajiwa kuangalia darasa zao zote kila JUMATATU (isipokuwa Jumatatu ni likizo, basi angalia Jumanne) kwa kuenda kwa Google Classroom au jukwaa la mbali ambalo mwalimu amegawa na wanafunzi. Kazi za nyumbani zinatakikana kila Ijumaa kabla ya usiku kucha isipokuwa imejadiliwa na mwalimu *mwisho wa siku ya shule Alhamisi*.
- Wanafunzi wanatarajiwa kujihusisha na kuwasiliana na walimu katika mbinu moja au zaidi ya mbinu zifuatavyo:
 - Kuhudhuria Google Meeting
 - Kuandika maoni katika mjadala wa mtandao au maandishi ya blog
 - Kuomba usaidizi/utegemezi kutumia chat au baruapepe
 - Kutoa mchango kupitia Google Classroom au baruapepe
- Wanafunzi wanatarajiwa kutoa angalau saa 3 kila siku kwa mafunzo ya mbali.
- Wanafunzi wanatarajiwa kukamilisha na kuwasilisha kazi zao za nyumbani za kila wiki siku ya Ijumaa ya kila siku. Wanaweza kuwasilisha kazi zao za nyumba katika mbinu zifuatazo, kulingana na maagizo kutoka mwalimu wao:
 - Google Classroom au jukwaa lolote lililoamuliwa na mwalimu
 - Baruapepe
 - Iwapo wanafunzi wanakumbana na shida kuwasilisha kazi, wanatakiwa kuwasiliana na mwalimu wao kwa mara moja na kuongojea mwongozo zaidi kutoka kwao.
- Wanafunzi wanaokumbana na shida isiyo ya kawaida katika zama hizi zisizotabiriwa wanafaa kuwasiliana na [Wakuu wa Kitivo za Nyumba](#) wao kupitia baruapepe ili kuunda mpanga unaoweza kutumika katika muda huu.

“SAA ZA OFISI” NA WALIMU KWA MAFUNZO YA MBALI

Ili kusaidia wanafunzi kujifunza kwa mbali na kufanya maendeleo katika kazi za nyumbani, walimu watapanga masaa ya ofisi ya kila siku ambayo yatawasilishwa kwa wanafunzi moja kwa moja. Wanafunzi na familia wanafaa kujua kwamba wanauwezo kila mara kufanya mazungumzo ya chat ya kibinafsi na walimu, kwa makubaliano yao.

JEE MATOKEO YA SEHEMU YA 3 YA MWAKA WA SHULE NA KIPINDI YATAAMULIWA KIVIPI?

Kwa sababu ya muda uliyopotea kati ya kufunga shule na kuanza mafunzo ya mbali, tumeamua kwamba haitakuwa katika faida ya wanafunzi iwapo tutakuwa na matokeo tofauti ya Sehemu ya 3 ya mwaka wa shule. Badala ya hivyo, tutatoa tokeo moja kwa kazi iliyofanyika kipindi nzima. Wanafunzi na familia wanafaa kuelewa kwamba Idara Huru ya Elimu Msingi na ya Upili imependekeza kwamba matokeo ya kipindi cha pili yatakua kufaulu/kuanguka (faulu/anguka) pekee. LHS kwa sasa inarejelea miongozo ya matokeo. Itakapokamilika, jamii itapata habari

Mraba kwa shule mzima ambayo inaonyesha namna wanafunzi watapata matokeo imeongezwa hapa chini.

Kumbukumbu: Masomo za MCC za Kujiandikisha Mara Mbili zitafuata miongozo zilizopo yaani tokeo la nambari kwa MCC. Kutoka Aprili tarehe 6, 2020 tunaendelea kutafuta mbinu ya kutekeleza hili na tutabadilisha hati hili na kuwajulisha wanafunzi tutakapoamua namna hili litatendeka.

MRABA WA MATOKEO

Lengo: Mwanafunzi aonyeshe ustadi kutumia kiwangongezi cha mafunzo katika majibu yake au kazi yake.

Masomo ya Ubinadamu na Sanaa – Sanaa za Lugha ya Kiingereza na Masomo ya Jamii, Lugha za Dunia, Sanaa za Ubunifu

STEM - Sayansi, Teknolojiya, Uhandisi, Hesabu (Biashara, Upishi, Afya)

PE na AFJROTC – utakuwa na mraba tofauti utakayopatiwa wanafunzi

MRABA WA MATOKEO - IKIENDELEA

Anatimiza Matarajio	Anatimiza Sehemu ya Matarajio	Rejelea na Wasilisha upya
<p>Masomo ya Ubinadamu Unaonyesha kujihusisha wa <i>kina</i> na kifaa na majibu zako ni kamili, zinazofaa, na sahihi.</p> <p>Jibu linatimiza au kupita tarajio katika yaliyomo na urefu, na matumizi ya lugha (sarufi, vituo na nokta, na namna).</p> <p>STEM Jibu zako ni sahihi na kamili, umejibu swali uliloulizwa.</p> <p>Kazi yote imeonyeshwa.</p>	<p>Masomo ya Ubinadamu Unaonyesha kujihusisha na kifaa na majibu zako zinafaa, na ni sahihi.</p> <p>Jibu liko kidogo chini ya kutimiza tarajio la yaliyomo na urefu.</p> <p>STEM Mengi ya majibu yako ni sahihi, ambalo linaonyesha kwamba una ufahamu fulani wa vifaa.</p> <p>Kiasi kikubwa cha kazi chako au fikra yako hakijaonyeshwa.</p>	<p>Masomo ya Ubinadamu Unaonyesha kujihusisha kiasi na kifaa lakini majibu yako si kamili na si sahihi.</p> <p>Jibu liko chini zaidi ya tarajio la yaliyomo na urefu.</p> <p>STEM Mengi ya majibu yako si sahihi, na huonyesha ufahamu ndogo wa vifaa.</p> <p>Umeonyesha kiasi kidogo sana au hujaonyesha kazi yoyote.</p> <p>Jibu linafaa kurejelewa na kuwasilishwa upya kuonyesha ufahamu wa kutosha wa ustadi na vifaa.</p>

JE NITAWASILIANA AJE NA MSHAURI WANGU WA SHULE?

Familia na wanafunzi wanaweza kuwasiliana na mshauri wao katika Masaa ya Ofisi na kutarajia jibu ndani ya masaa 24. Washauri pia wanaweza kupatikana na wanafunzi ili kusaidia wanafunzi wao na kujibu maswali na wasiwasi wa walimu na wazazi kutumia baruapepe ndani ya siku nzima.

Mshauri	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa
Mendonca	12-1	12-1	12-1	12-1	12-1
Boisvert	2-3	2-3	2-3	2-3	2-3
Griffin	11-12	11-12	11-12	11-12	11-12
Sarin	9-10	9-10	9-10	9-10	9-10
Uong	2-3	2-3	2-3	2-3	2-3
Figueroa	9-10	9-10	9-10	9-10	9-10
Crowell	1-2	1-2	1-2	1-2	1-2
Devost	10-11	10-11	10-11	10-11	10-11
Cassidy	1-2	1-2	1-2	1-2	1-2
Blouin	11-12	11-12	11-12	11-12	11-12
Brunner	8-9	8-9	8-9	8-9	8-9
Ribaudo-Smith	8-9	8-9	8-9	8-9	8-9

Meng	12-1	12-1	12-1	12-1	12-1
------	------	------	------	------	------

RASILIMALI ZA KIJAMII NA KIHISIA:

Wakati wa kufunga shule, Washauri wa LHS Counselors na Wafanyikazi wa Jamii wataweza kupatikana kupitia baruapepe kwa maswali na wasiwasi unazoweza kuwa nazo na pia kupanga mkutano katika masaa ya ofisi. Lakini, tafadhali kumbuka kwamba iwapo kuna mahitaji au mgogoro ya afya ya akili baada ya masaa ya shule, tafadhali fikiria kutumia rasilimali zifuatazo au pigia 911 mara moja.

Leahy Health

<http://nebhealth.org/services-locations/emergency-psychiatric-care-mobile-crisis-team/>

Lowell Community Health Center

<https://www.lchealth.org/patients/connect-services/behavioral-health-services>

Bridgewell

<https://www.bridgewell.org/behavioral-health-services/outpatient-clinics/bridgewell-counseling-services-lowell/>

Mfanyikazi Wa Jamii	Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa
Correa	9:30-10:30	9:30-10:30	9:30-10:30	9:30-10:30	9:30-10:30
Martel	8-9	8-9	8-9	8-9	8-9
Quattrocchi	11-12	11-12	11-12	11-12	11-12
Ricciardi	2-3	2-3	2-3	2-3	2-3

Hosmer	10-11	10-11	10-11	10-11	10-11
Schwartz	1-2	1-2	1-2	1-2	1-2
Bernstein	12-1	12-1	12-1	12-1	12-1

KWA WALIMU

MATARAJIO YA WALIMU:

- Walimu wataendelea kushughulikia na miungano na wanafunzi.
- Walimu watapea kazi za nyumbani za wiki kila Jumatatu na wanaweza kutumia Google Classroom au jukwaa lingine watakaochagua kwa mawasiliano na mafunzo inapofaa. Kazi zote za nyumbani ni lazima ziweze kufanyika na simu ya mkono na haziwezi kutaka wanafunzi kuchapisha ili kukamilisha kazi.
- Walimu watatoa kazi ya saa 2.5 ya kazi ya shule kila wiki (dakika 25 kwa siku) kwa kila darasa
- Walimu watawasiliana kila siku “Saa zao za Ofisi”
- Walimu wataongoza mafunzo ya wanafunzi kulingana na mtaala uliyo kwa mtandao uliyotolewa na mtaa panapofaa, na kuongezea na video na vifaa vingine inavyohitajika.
- Walimu watarekodi mawasiliano yao na wanafunzi kila wiki na mwenyekiti wa idara.
- Walimu watalinda vitabu vya matokeo na watarekodi kazi ya marejeleo ili kurejesha matokeo na kusaidia kutimiza matarajio ya kuhitimu.
- Walimu wataendelea kuwasiliana mara kwa mara na wanafunzi/wazazi kupitia mbinu ya mawasiliano wanayopendelea zaidi. Walimu watatumia anwani ya baruapepe ya shule.
- Walimu wanatakiwa kujibu baruapepe za wanafunzi/wazazi/wasimamizi ndani ya masaa 24.
- Walimu watafuatilia maendeleo ya mwanafunzi na kutoa maoni katika muda mwafaka kwa wanafunzi.
- Walimu wanafaa kutumia wanafunzi na/au wazazi/walezi wakati mwanafunzi hafanyi mawasiliano na hajihusishi na kazi. Iwapo hakuna jibu kutoka

mwanafunzi baada ya kufuata nidhamu ya mawasiliano kabla ya Jumatatu, Aprili 13 basi mwalimu anafaa kuwasiliana na nyumba ya ofisi ya mwanafunzi. Wafanyikazi wa nyumba ya ofisi, mtu wa mawasiliano na wazazi na walimu watafuatilia.

- Walimu watawapatia nafasi zaidi iwezekanavyo wanafunzi walio kwenye programu za IEP. Walimu watawasiliana na msimamizi wa kesi ya Elimu Maalum iwapo usaidizi au ufafanuzi unahitajika kuhusu utoaji wa nafasi zaidi.
- Walimu, washauri wa shule, na watoa huduma wanaohusika watahudhuria mikutano ya mbali ya IEP kwa wanafunzi wa elimu maalum katika darasa zao. Iwapo hawataweza kuhudhuria, watahitaji kukamilisha fomu iliyoambatanishwa na mwaliko wa mkutano ili kutoa maoni kabla ya mkutano.

KWA USIMAMIZI WA UONGOZI WA KIUTAWALA

MATARAJIO YA UONGOZI:

- Wasimamizi wako ili kusaidia walimu na kujibu maswali na wasiwasi walizo nazo wanafunzi na wazazi; tafadhali panga wakati maalum ili kupiga simu, itakapohitajika. Unaweza kuongoja jibu kupitia baruapepe ndani ya masaa 24.
- Wasimamizi watapanga mikutano ili kujadili maendeleo na maswali na wafanyikazi wao, inavyohitajika.
- Wasimamizi watahudhuria mikutano ya mara kwa mara ya Uongozi wa Timu ili kujadili maendeleo na maswali yanayohusu ufungaji wa shule na Mpango wa Mafunzo ya Mbali.
- Wasimamizi watawapatia walimu mafunzo kwa walimu watakaomba usaidizi ili kufunza inavyotakikana.
- Wasimamizi wataendelea kushughulikia Mpango wa Kugeusha Shule na kusaidia Timu la Uongozi wa Elimu.